



## **TANGAZO KWA UMMA**

### **BENKI KUU YA TANZANIA YACHUKUA USIMAMIZI WA BANK M TANZANIA PLC**

Kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha sheria namba 56(1)(g)(iii) cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, Benki Kuu ya Tanzania imeamua kuchukua usimamizi wa Bank M Tanzania Plc (Bank M) kuanzia tarehe 2 Agosti 2018.

Uamuzi huu umechukuliwa baada ya kubaini kuwa Bank M ina upungufu mkubwa wa ukwasi kinyume na matakwa ya sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na kanuni zake. Upungufu huu wa ukwasi unahatarisha usalama wa sekta ya fedha na pia kuendelea kutoa huduma za kibenki kwa Bank M kutahatarisha usalama wa amana za wateja wake.

Kutokana na uamuzi huo, Benki Kuu ya Tanzania imeisimamisha Bodi ya Wakurugenzi na uongozi wa Bank M kuanzia tarehe 2 Agosti 2018. Kufuatia uamuzi huo, Benki Kuu ya Tanzania imemteua Meneja Msimamizi ambaye atakuwa na jukumu la kusimamia shughuli za Bank M kwa kipindi ambacho itakuwa chini ya usimamizi wa Benki Kuu. Pia, umma unaarifiwa kuwa katika kipindi kisichozidi siku tisini (90) kuanzia siku ya taarifa hii, shughuli za utoaji wa huduma za kibenki za Bank M zitasimama ili kuipa nafasi Benki Kuu ya Tanzania kutathmini hatua za kuchukua ili kupata ufumbuzi wa suala hili.

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuuhakikishia umma kuwa itaendelea kulinda maslahi ya wenye amana katika mabenki kwa lengo la kuleta ustahimilivu katika sekta ya fedha.

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**2 Agosti, 2018**